

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
9 August 2008**

**Waliohudhuria**

Ally Athuman Jumbe  
Amar Shanghavi  
Aseli Wilison  
Bashiri Rashidi  
Dominata Rwechungura  
Edgar R Paulo  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Frank Peter Rwechungura  
Fredy H Lwila  
George Kabogo  
Juma Hassan Chibaya  
Juma Imori Rugole  
Juma Ali Salehe Jongo  
Mussa Alex  
Nickson Kilunga  
Paulo Atibu Hatibu  
Pendo January  
Shukuru Hassan

**Magazeti**

Ally Athuman alileta makala ya Alhasiri inayohusika usalama wa baisikeli na inataja TANROADS na UWABA. Wanachama wengine pia walileta makala yanayohusika baisikeli. Tulikubaliana kuwa na faili ofisini kuhifadhi magazeti yanayohusika baisikeli.

**gTKP**

Elaine alisema alimtumia email kwa Stephen wa gTKP kufuatalia mkutano wa wiki ijayo na anatumaini kupata jibu.

**Ofisi**

Shukuru alileta taarifa kwamba kuna bao nyeusi zinapatikana kwa Tsh 25,000, Tsh 35,000 au Tsh 56,000 kwa kutegemea ukubwa. Hizi ni rahisi kuliko zingine basi tulikubaliana kwamba yeye na Juma waende kununua bao mbili ndogo jumatatu.

Ofisi bado haina nembo ya rangi kwenye ukuta.

## **Mradi wa usalama barabarani - Wamba Memorial Fund na video ya kufundisha**

Wanachama walipenda wazo la Amar kutengeneza video ya kufundisha usalama wa baiskeli ambayo tunaweza kuwapa watu wa TV stations. Kwa sababu Amar atakuwepo hapa kwa wiki tatu zaidi tulikubaliana kwamba tutengeneze video baada ya wiki mbili (tarehe 23 August). Elaine atawauliza chuo cha usafirishaji kama tunaweza kutumia uwanja wao. Mpango wa video ni kama ifuatavyo:

- Uhandisi, Elimu, Utekezaji wa Sheria, Mazingira na Uhamasishaji – wanachama mbali mbali
- Sehemu za baiskeli na kazi zao – Ally Athman
- Kukagua baiskeli yako, saizi ya baiskeli, kuvaa helmeta – Dominata na Frank Peter
- Uendeshaji salama wa baiskeli
  - Kupanda baiskeli yako na kuanza safari – Bashiri
  - Kuendesha wapi (upande wa kushoto, service roads)
  - Kuwa makini kuangalia na kusikia
  - Kukamiliki baiskeli yako – Aseli
  - Kupita (mfano watembea kwa miguu, mashimo, wapanda baiskeli wengine)
  - Alama za mikono
  - Alama za barabarani – Filbert
  - Makutano - Edgar

## **Mkutano wa kila mwezi**

Tuliamua kuandika barua kuwaalika TANROADS, serekali ya jiji na traffic police kwenye mkutano ofisi ya UWABA ambapo tunaweza kuongea kuhusu mikutano ya kila mwezi.

## **Rais Kikwete**

Elaine aliandika barua kwa Rais Kikwete na wanachama walipitia na Filbert alisahihisha.

Paulo alienda Radio Tanzania halafu TBC ambao walisema tunaweza kupata audio tape ya hotuba ya Tanga kwa Tsh 5,000, CD kwa Tsh 25,000 au video kwa Tsh 50,000 lakini lazima tsubiri mpaka waandishi wa habari wanarudi ofisini na watawasiliana nasi.

## **Msafara wa Baiskeli**

Elaine aliongeza T-shirts kwenye proposal kama tulivyokubaliana wiki jana. Alileta barua ubalozi wa Ireland, ubalozi wa Uholonzi, kampuni ya guta na kampuni ya Bakhrasa na hizi zilisemekwa na wanachama. Kwa Bakhrasa tulikubaliana kuongeza kuomba bites pamoja na maji ya kunywa. Juma atatembelea maofisi na barua tatu wiki hii. Wanachama walipendekeza pia tuwasiliana na Vodacom (ambapo Amar anamfahamu mtu ataweza kutusaidia), kampuni zingine za simu, CRDB (ambao juzi juzi walitoa baiskeli kama zawadi kwenye mashindano ya maths ya shule za Dodoma), NMB (benki yetu), Ulitimate Security na Irish pub.

Amar alisema kwamba anajua wapi helmet zinapatikana kwa Tsh 10,000 ya bei ya ujumla na pia ataweza kutafuta bei za ujumla kwa baiskeli tukipata wadhamini wa kifedha kununua vitu hivi.

### **Kupiga round kila wiki**

Tulipiga round kwa baiskeli Manzese na watu walituona na wakauliza kuhusu UWABA. Tulikubaliana kutafuta njia nzuri zaidi wiki ijayo na tuhakikisha kutoa mfano mzuri kwa kuonyesha alama za mkono n.k..

### **Vipeperushi**

Paulo, Aseli na Shukuru wote walichukua vipeperushi ili kubadilisha sehemu ya ofisi iliandikwa pale.

### **Mambo ya hela**

Juma alibaki na Tsh 13,300 kutoka hela ya guta kabla ya mkutano. Pia alikuwa na Tsh 64,850 kutoka hela ya Wamba. Jumla ni Tsh 78,150. Tulitoa posho ya julai na agosti ili abaki na Tsh 38,150.

Filbert alileta Tsh 21,000 ya hela ya guta iliyotumwa na Ally Saidi Mwishehe kwenye mkutano na hela hiyo tulimpa Tsh 21,000 kwa Shukuru na Juma ataleta hela zingine ili wanaweza kununua bao za tangazo wiki hii.

### **Mambo mengine**

Edgar alipata t-shirt ambapo ina maneno “No Iraqis were killed to fuel this bicycle” alipata wazo kutoka t-shirt ya Andrew ambayo wanachama wote walipenda.